# ***JIFUNZE KINANDA HATUA YA KWANZA, Na. Sabas Patrick.***

Mimi ni **Sabas Patrick** kutoka Kyerwa- Kagera-Tanzania. Nachukua nafasi hii muhimu kukukaribisha katika ulimwengu unaovutia wa kucheza kinanda.
Kama kweli upo tayari na unapenda kutumika kama mpiga kinanda kanisani, MAKALA hii itakupatia zana zitakazo kusaidia wewe kujiamini katika kukuza kipaji chako kwa hatua hii ya kwanza.

Kwanza kabisa, ujuzi unaohitajika katika kutumia makala hii ni kuwa na msingi tu kwenye Nadharia ya Muziki yaani kusoma na kuandika nota, pia kuelewa, kuchambua na kusikiliza muziki. Kama bado, chukua muda kidogo angalau kujua Tempo na Thamani za Nota tu, ili uweze kupata wepesi wa kuzingatia mazoezi yaliyotumika katika MAKALA hii.

Kujifunza kupiga kinanda ni safari ndefu na pana kama ilivyo katika kujifunza Muziki wenyewe. Mara nyingi wengi hutamani au hupenda kujifunza kinanda lakini wanashindwa kwasababu ya kukosa msaada. Hivyo, nimepata msukumo wa kuandaa MAKALA hii itakayoweza kutupatia mwanga katika kujifunza kinanda kwa hatua hii ya kwanza.
Aidha katika MAKALA hii nimeweka kanuni msingi za mwanzo anazotakiwa mpiga kinanda azijue kadri anavyo endelea kujifunza kinanda. Tujitahidi sana kuzingatia kanuni hizi kwa moyo naamini zitatusaidia.

Mwisho, tukumbuke kila somo la Muziki ni kubwa sana. MAKALA hii ni jitihada ndogo tu katika kumsaidia mwanafunzi anayejifunza kinanda kwa hatua ya kwanza, hivyo kwa upendo mkubwa nakaribisha maoni, marekebisho na masahihisho.

Kwa wote tutakaotumia MAKALA hii, ili kukuza kipaji chako ni muhimu sana kwenda taratibu na kubaki katika lengo, kujiamini na endelea kujifunza. Nakutakia kila lenye heri katika safari zako za kujifunza Muziki popote pale zitakapoelekea. Asante!

**MAWASILIANO**
**SIMU:** 0757341313 (WhatsApp) na 0712229496
**Email:** sabaspatrick1@gmail.com au patricksabas32@yahoo.com

***JIFUNZE KINANDA HATUA YA KWANZA, Na. Sabas Patrick.***

## *SURA YA KINADA

-Kama inawezekana, ni vizuri ukipata MAKALA hii tafuta kianda kidogo cha mezani (portable) cha kufanyia mazoezi.

-Kinanda kina batani za aina mbili yaani nyeupe na nyeusi.

-Batani nyeusi zipo kwenye makundi ya mbili kwa tatu, na hutumika katika kutafuta funguo.

-Batani nyeupe ya kwanza kutoka mkono wa kushoto kabla ya batani nyeusi mbili ni noti "do" ya ufunguo C. Tukihesabu batani nyeupe tu kwa kupanda tutakuta noti ya nane (8) inafanana na hiyo ya kwanza.

-Batani nyeupe (8) zinaunda ngazi ya ufunguo C ambao ni ufunguo mama kwa funguo kubwa zote 7 (major keys), yaani DO RE MI FA SO LA TI (C D E F G A B)

-Ili kupata ngazi kubwa yoyote kwenye kinanda iwe D E F au G. Gusa batani ya ngazi unayohitaji, mfano G ndio itakuwa "do" ya ngazi kubwa ya G. Kutafuta "re, mi, fa, so, n.k kwenye ufunguo huu wa G, ni kwamba kila batani mbili zilizofuatana ziwe nyeupe au nyeusi zinahesabu moja. Kwahiyo, tutahesabu 1 2 3 na 1/2, 1 2 3 na 1/2 yaani G A B na C, D E F# na G ambazo ni "DO RE MI FA SO LA TI DO" za ufunguo G kubwa.

-Pia ngazi kubwa ya D ni "D E F# G A B C# D". Kumbuka alama (#) inaelekeza tucheze batani nyeusi siyo nyeupe katika ngazi husika. Kumbe kuna batani nyeusi 1 kwenye ufunguo G, nyeusi 2 kwenye ufunguo D, n.k

-Jaribu sasa kutafuta ngazi kubwa za A, E, B na F.

## *MPANGILIO WA VIDOLE (Fingering)

-Ili kujifunza kupiga kinanda, hatua ya kwanza ni kujifunza kupanga kidole kimoja kimoja.

-Kwa kila mkono (kushoto au kulia) vidole jumla yake ni tano (5). Tunaanza na kidole Gumba (1) hadi cha mwisho (kadogo) ni namba 5.

### +Mazoezi ya kulainisha vidole

-Anza na mkono wa kulia, kisha wa kushoto, halafu changanya mikono yote kwa pamoja.

-Anza na mapigo ya Minim (nusu noti), fuatia Crotchet (robo noti), fuatia Kinane na Nusu kinane.

**NGAZI KUU YA C (Ufunguo C)**


-Tutaanza na kidole kimoja kimoja

-Fanya mazoezi kwa kufuata Tempo na Thamani za nota

-Hakikisha unapanga vidole vyako vizuri, kila kidole na batani yake

++***Kwa kila zoezi, anza na mkono mmoja mmoja, halafu ukielewa changanya yote kwa pamoja.***


**1. (a). Mkono wa Kulia- Kupanda na Kushuka**




**(b). Mkono wa Kushoto- Kupanda na Kushuka**





**2. (a). Mkono wa Kulia**




**(b). Mkono wa Kushoto**





**3. (a). Mkono wa Kulia**





**(b). Mkono wa Kushoto**




**4. (a). Mkono wa Kulia**




**(b). Mkono wa Kushoto**




**(c). Mikono yote kwa Kupanda na Kushuka**




## ***KUPIGA KINANDA**

Katika kupiga kinanda, kwenye MAKALA hii tutajifunza juu ya Muziki Mtakatifu wa Kanisa Katoliki unaoandikwa kwa kodi ya nota nne, wenye sauti nne, yaani Soprano (I), Alto (II), Tenor (III) na Bass (IV).

Ambapo Soprano (I) na Alto (II) hujitokeza kwenye G-Clef, Tenor (III) na Bass (IV) kwenye F-Clef. Lakini mara nyingine Soprano (I), Alto (II) na Tenor (III) hujitokeza kwenye G-Clef na Bass (IV) kwenye F-Clef.

Hivyo, kutokana na mwingiliano huu tunapata kanuni mbili za mpangilio wa vidole (fingering) zitakazotumika katika MAKALA hii.

**-Tunatumia namba zilezile za vidole katika kujifunza kanuni hizi muhimu.**


### **1. Kanuni ya Tatu kwa Moja**

Katika kanuni hii, mkono wa kulia unacheza sauti tatu: Soprano (I), Alto (II) na Tenor (III) na mkono wa kushoto sauti moja ya Bass (IV). Hii kanuni ilitumika tangu zamani kidogo kwasababu hapo mwanzo mpangilio wa kodi zenye nota nne katika "stave" ulikuwa tatu kwa moja.

+**Mpangilio wa vidole**

Kuwa makini, panga vidole vizuri ili usiharibu batani za kinanda na jaribu kuondoa ugumu katika kuhamisha vidole. Katika kanuni hii tutaishia kwenye mpangilio wa vidole.

-Fanya zoezi hili kwa kupanda tu.




## 2. Kanuni ya Mbili kwa Mbili


Hii kanuni ni muhimu na nzuri sana kwasababu inasaidia mpiga kinanda kucheza sauti zote kama zilivyo andikwa na mtunzi kwenye wimbo.

- Fanya mazoezi yafuatayo katika funguo zote kubwa (major keys) kwa kupanda na kushuka.


-Anza na mkono wa kulia, fuatia wa kushoto na kisha changanya mikono yote kwa pamoja.

-Zingatia Tempo na Thamani za nota.

***(a). Mikono yote- Kushuka***



***(b). Mikono yote- Kupanda***





****BAADHI YA MAZOEZI MUHIMU**

Nyimbo nyingi nzuri za Muziki Mtakatifu zilizotulia na kuandikwa vizuri zenye tafakari, zinapendeza zikichezwa kwenye kinanda kama zilivyoandikwa na watunzi bila kuacha nota hata moja.

Yafuatayo ni baadhi ya Mazoezi Msingi katika hatua za kukokotoa (ku-solve) nyimbo za Muziki Mtakatifu. Tutatumia funguo kubwa tatu yaani C, G na A. Lakini, cheza mazoezi haya katika funguo zote kubwa (major keys).


**(a). Ufunguo C**



**(b). Ufunguo G**



**(c). Ufunguo A**



****MUHIMU!**

Mpiga kinanda ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

1. Tempo, Alama za Nyakati na Thamani za nota uzijue vizuri
2. Epuka usahaulifu
3. Kuwa na Nidhamu
4. Kujua kusoma Muziki vizuri (Sight reading)
5. Kuwa na Sikio la Muziki (Ear training)
6. Kuendelea kufanya Mazoezi mengi na kupanga vidole vizuri
7. Jitahidi kukokotoa (ku-solve) nyimbo nyingi, yaani kucheza wimbo jinsi ulivyo.

\- **Mfano:** Jifunze nyimbo zifuatazo:-

(a). Kutoka katika Kitabu cha "Nyimbo za Liturjia" cha mwaka 1994 (Namba Moja)

(1) Nitajongea meza yako (uk. 819)

(2) Tunakushukuru Bwana (uk. 841)

(3) Tunakushukuru Mama Maria (uk. 866)

(4) Bwana Yesu ni chakula (uk. 796)


(5) Salamu Maria (uk. 861). Huu upo G, ila uweke A.

(b). Kutoka kwa baadhi ya Watunzi


(1) Mezani pake (Na. F.A.Nyundo)
(2) Pokea ombi letu (Na. Fr.G.Kayetta)
(3) Msaada wangu (Na. Sabas Patrick)
(4) Ekaristi chakula cha uzima (Na. Fr.John Msamire)
(5) Sadaka yangu Ee Bwana (Na. Fr.Amedeus Kauki)

(c). Kati ya hizi nyimbo (10) kutoka (a) na (b) hapo juu, nimekokotoa nyimbo (3) tu. Hakikisha unakokotoa hizo (7) zilizobaki.


**NITAJONGEA MEZA YAKO**



**MSAADA WANGU**



**SALAMU MARIA**



## SHUKURANI

Shukurani zangu za dhati ni kwake Mwenyezi Mungu muweza wa yote, anayetukirimia kila wingi wa neema na baraka. Naishukuru familia yangu: mke wangu mpenzi ATUBELA MTAFUNGWA, mwanangu mpendwa ANIELA SABAS na wazazi wangu wapendwa Bw. na Bi. PATRICK MICHAEL pamoja na wadogo zangu wote, asanteni sana kwa upendo wenu.

Pia shukurani zangu za pekee ni kwa walimu wangu na marafiki zangu katika taaluma hii ya Muziki Mtakatifu, baadhi yao ni hawa wafuatao: Fr. Alistides Danda, Dr. Alex X. Matofali, Ernest Bilega, Deusidedith Bahela, Edward Kaniki, Boniface Massawe, Lusekelo Haonga, Izdory Kunambi (Apumzike kwa amani), Joseph Waziri, Francis Patrick, Emmanuel Mgwayah, Godfrey Kasanda, Charles Kadudu, Michael Marenge; na wengine wote tuliowahi kushirikiana kwa namna moja au nyingine, ambao sikuweza kuwataja katika MAKALA hii, nawashukuru sana.